

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA KWANZA**

**02 APRILI, 2024**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 02 APRILI, 2024**

**I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:**

**II. DUA:**

**III. TAARIFA YA SPIKA:**

**IV. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI MKUU:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## **V. MASWALI:**

### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **1. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Shitage - Uyui kilichoanza kujengwa kwa nguvu za Wananchi.

#### **2. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ahadi yake ya kuifanya Zahanati ya Solwa iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kuwa Kituo cha Afya.

#### **3. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatangaza maeneo mapya ya kiutawala.

**4. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka Walimu wa kutosha katika Shule mpya kumi za Msingi na Sekondari zilizojengwa - Vwawa.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**5. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini Serikali itawasilisha Marekebisho ya Sheria ya Mazingira ili kuipa NEMC uwezo na hadhi ya Mamlaka.

**WIZARA YA KILIMO:**

**6. MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imefanya utafiti kubaini sababu zilizosababisha Wakulima kupata hasara katika mavuno ya Mwaka 2022/2023.

#### **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

##### **7. MHESHIMIWA ALEKSIA ASIA KAMGUNA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupanda miti katika Mkoa wa Morogoro hususani Milima ya Uluguru na kandokando ya Mto Fulua, Mnyera na Kilombero.

#### **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

##### **8. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mkalama utaanza.

## **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

### **9. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, kuna mpango gani wa kuyafanya mafunzo ya Mgambo kuwa sehemu ya mafunzo kwa Vijana wanaokosa nafasi ya kujiunga na JKT.

## **WIZARA YA UCHUKUZI:**

### **10. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa Bandari Kavu utaanza katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma.

### **11. MHESHIMIWA DKT. ANGELINE SYLVESTER LUBALA MABULA (ILEMELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini mgogoro kati ya Wananchi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - Mwanza utatatuliwa.

## **WIZARA YA AFYA:**

### **12. MHESHIMIWA TAUHIDA CASSIAN GALLOS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha Sera ya Wazee kupata matibabu bure inatekelezwa katika kila Kituo cha Afya nchini.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **13. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Bukumbi - Meatu.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **14. MHESHIMIWA JEREMIAH MRIMI AMSABI (SERENGETI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya lami kipande cha Sanzate hadi Natta.

**WIZARA YA FEDHA:**

**15. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA  
(CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, sababu gani zilisababisha maduka ya kubadilisha Fedha kuondolewa katika biashara na Wananchi wengi kupoteza ajira zao.

**DODOMA  
02 APRILI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**

